**25 APRILI, 2022**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 25 Aprili, 2022**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. NENELWA MWIHAMBI, *ndc* – KATIBU WA BUNGE:**

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa masikitiko makubwa naomba kuwatangazia kifo cha Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Rukwa kupitia Chama cha Mapinduzi ambaye alifariki jana Jumapili, tarehe 24 Aprili, 2022 katika Hospitali ya Tumbi, Kibaha alipokuwa anapatiwa matibabu.

Mheshimiwa Ndyamkama aliugua ghafla akiwa safarini kuelekea Dar es Salaam na akalazimika kukimbizwa hospitalini kwa matibabu ya haraka.

Naomba kutumia fursa hii kutoa pole kwa familia ya marehemu, ndugu, jamaa, wananchi wa Mkoa wa Rukwa na Waheshimiwa Wabunge wote.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni na utaratibu wetu, tunapofiwa na Mbunge mwenzetu wakati wa Mikutano ya Bunge siku ya kazi kunakuwa hakuna kikao cha Bunge ili kupata fursa ya kuomboleza msiba huu na kujiandaa kuupokea mwili wa mwenzetu.

Kufuatia msiba huu, taarifa za awali ni kwamba mwili wa marehemu utaletwa Bungeni siku ya Jumatano, tarehe 27 Aprili, 2022 kwa ajili ya kuagwa na mazishi yanatarajiwa kufanyika siku ya Ijumaa, tarehe 29 Aprili, 2022 Mkoani Katavi. Taarifa kuhusu msiba huu na jinsi tutakavyomuaga mwenzetu zitaendelea kutolewa.

Baada ya kuyasema hayo niwaombe Waheshimiwa Wabunge tusimame wote kwa dakika moja kwa ajili ya kumpa heshima Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama.

(*Wabunge walisimama kwa muda mfupi ili kumuombea Mheshimiwa Marehemu Irene Alex Ndyamkama)*

**SPIKA:** Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Marehemu mahali pema peponi, amina.

Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, kufuatia hili ambalo nimelisema hapa niwaombe Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Bunge pamoja na Wajumbe wa Kamati ya Uongozi baada ya kuahirisha shughuli za Bunge tutakuwa na kikao kwenye Ukumbi wa Spika hapa nyuma.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba huwa hatufanyi shughuli za Bunge ama shughuli zozote siku ya leo,

lakini hapa Bungeni tunao wageni ambao wapo, kwa hiyo, mniruhusu niwatangaze.

Tunao wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge na wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; tunao wageni 44 wa Mheshimiwa Michael Mwakamo ambao ni Wanakwaya wa Kristo Mfalme kutoka *RC* Mlandizi, Mkoa wa Pwani, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni watano wa Mheshimiwa Rehema Migilla ambao ni rafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam, pengine hawajapata fursa ya kuingia humu ndani.

Wageni saba wa Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati ambao ni Wajumbe wa Halmashauri ya Vijana wa Kanisa la KKKT kutoka mikoa mbalimbali wakiongozwa na Mratibu wa Vijana KKKT, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni 53 wa Mheshimiwa Venant Daud ambao ni watumishi na wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Trifa wakiongozwa na Mwenyekiti wa Bodi ya Shule, Mheshimiwa Makoba Lubasha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo na kuna mgeni mmoja kutoka *TANFORM Ltd.* ya Arusha ambao ni wazalishaji wa magodoro ya aina mbalimbali Ndugu Omary Koshuma. *(Makofi)*

Naambiwa hawa *TANFORM* pia wapo hapa viwanja vya Bunge kwa ajili ya kuonesha bidhaa zao. *(Makofi)*

Wapo pia walimu na wanafunzi 65 kutoka Shule ya Sekondari Mjimpya ya Morogoro Mjini, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi na walimu 10 kutoka shule ya wanafunzi wenye mahitaji maalum, *Al Muntazir Special Education Needs* ya Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na

Mkuu wa Shule hiyo Mwalimu Zaida Chagani, karibuni sana, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 25 na walimu sita kutoka Shule ya Msingi ya Mtakatifu Gasper ya Jijini Dodoma wakiongozwa na Mwalimu Panga Faustine, karibuni sana. *(Makofi)*

Lakini pia yupo Mwinjilisti Nicolaus Fungameza kutoka Jijini Arusha, ahsante sana. *(Makofi)*

Niwaombe tena Wajumbe wa Tume na Wajumbe wa Kamati ya Uongozi tukutane kwenye ukumbi hapa nyuma.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo na kuwaeleza taratibu zetu zilivyo kikanuni, basi naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatano, saa tatu kamili asubuhi.

(*Saa 3:07 asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano, Tarehe 27 Aprili, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*